Coptic Orthodox Patriarchate
His Holiness Pope Tawadros II
Pope of Alexandria and
Patriarch of the See of St. Mark
The Papal Center

بطريركية الأقباط الأرثوذكس
قداسة البابا الأنبا تواضروس الثاني
بابا الأسكندرية
وبطريرك الكرازة المرقسية
المقر البابوي

222 Ramses St., Abbaseya, Cairo, Egypt
Tel: 024822580 Fax: 0235365880 email: office@popetawadros.org

222 شارع رمسيس ، العباسية ، القاهرة ، مصر
تليفون: 024822580 فاكس: 0235365880

Swahili - 2020

Ujumbe wa Papa wa Siku Kuu ya Krismasi

Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu Mungu moja, Amina.

Nawapongeza wapendwa kwa huu mwaka mpya wa elfu mbili na ishirini, na kwa siku kuu ya uasili/kuzaliwa, ambayo tunakaribisha kuzaliwa kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye aliuchukua mwili wa binadamu kwa ajili ya kumkomboa mwanaadamu. Nawapongeza wapendwa wote katia kila dayosisi, na kwa makanisa yote ya Coptic Orthodox duniani nzima. Nawapongeza makasisi, metropolitani, maaskofu na mapadre, na mashemasi wote na waimbaji na wanaCoptic wote. Nawapongeza pia vijana, watoto na wazee. Nawatakia kila la heri ya mwaka mpya kila mara.

Katika sherehe kuu ya Uzalio, tunayoadhimisha kila mwaka na kuiweka katika kalenda yetu tukiitaja kuwa “Mwaka wa Bwana,” tunakumbuka mambo mengi kwa hayo. Kati ya maonyesho ya Kuzaliwa ni wakati Mamajusi walipokuja kutoka Mashariki na wakatoa zawadi tatu. Zawadi hizo tatu zinaashiria maisha ya mtu, maisha yake inayo nyakati za dhahabu, manemane na ubani. Hata hivyo, kupitia kuzaliwa kwa Bwana wetu, Yesu Kristo, na tukio zake, Mungu anatutolea zawadi tatu. Anatupa zawadi nyingi tunayoyaona katika matukio ya siku kuu ya Kuzaliwa. Zawadi hizi zinatolewa na Mungu kwa wanadamu ili kurejesha uwanadamu wake. Kwa uwanadamu, ambaye mwanadamu anakuwa, ni yathamani sana. Kwa kila sherehe ya Kuzaliwa, tunakumbuka lengo tatu ambayo nitaangazia.

Kwanza ni: Utu hufikiwa kama watu wanaishi pamoja kwa upendo. Ikiwa mtu anatenda, anaishi, na kutoa huo upendo, ni njia ya kutimiza utu wake. Ningependa kutaja onyesho fulani tunayopenda sisi sote, ni wachungaji kuishi maisha ya chini na ya unyenyekevu kwenye kiwanja, wakikesha kuangalia wanyama zao usiku kucha, huku waliishi kwa upendo – upendo kwa wanyama zao na upendo kwa wanadamu. Mungu aliwaamini kwa kuwafanya wakwanza kupata Habari Njema ya Kuzaliwa. Malaika aliwatokezea na kuwapongeza akisema: “Nawaleteni Habari Njema ya furaha ambae itakuwa ya watu wote (Luka 2:10). Hao wachungaji waliishi na kwa kutoa upendo. Walipopata ujumbe kwa malaika, walikwenda kwa haraka horini katika Bethlehemu. Walifurahi sana walipomuona Mtoto horini na wakaonyesha upendo wao mkuu katika tembezi hilo. Kwetu sisi, hiyo ilikuwa funzo wa kuonyesha upendo, na wanadamu waweze kuishi maisha ya upendo kila wakati.

Zawadi ya pili tunaona wakati mamajusi walipomtembelea Mtoto Yesu. Mamajusi walikuwa wageni kutoka Mashariki. Walikuwa wasomi wa nyota. Walipoona nyota ya kipekee angani, wakagundua kwamba ilikua ni ishara ya kuzaliwa kwa Bwana wa Ukweli.

Walifurahia kutenda mema, waliazimia kwa bidii ili waweze kupata mahali Kristo alipozaliwa kwa kufuata nyota, ndipo wakatoa zawadi nzuri. Walitokea Mashariki, wakakutana na mfalme, wakafika horini, kasha wakatoa zawadi zao. Hayo yanaonesha kuwa walifurahia kutenda mema na kutoa zawadi nzuri. Walifanya mema walipokuja na kutembelea Mtoto, na kutoa zawadi zao za dhahabu, ubani na manemane. Lakini katika eneo hilo, onyesho la tendo nzuri na binadamu, tunakumbuka watu wa Bethlehemu pamoja na wenye horini. Walimpokea huyu mama maskini, mama yetu, Bikira Mtakatifu Mariamu pamoja na Mtakatifu Yusufu mseremala. Mariamu alikuwa mjamzito na kuhitaji kumza Mwanawe. Nafasi haikupatikana katika mji huo mkubwa wa Yerusalemu, wala hata kijijini isipokuwa katika horini tu. Watu hawa wote walfanya mema. Kwa hivyo, zawadi ya pili nakutolea ni kujifunza kutenda mema kila wakati, kama vile tunamwambia Mungu: “Tumshukuru Mungu muumba wetu….

Zawadi ya tatu tunayoishuhudia ni kuonja uzuri. Uzalio wa Yesu Kristo ni mtazamo mzuri ambapo tukio zuri kuliko yote ilikuwa ni kwaya ya malaika wakitokea mbinguni na kuimba, kukariri na kukiri: “Atukuzwe Mungu juu mbinguni na duniani iwe Amani kwa watu aliowaridhia.” (Luka 2:14). Huu wimbo na kujieleza kwa furaha ilikuwa moja kati ya uzuri. Uzuri ni tabia yenye nguvu ambayo inashuhudiwa na wale wanaoishi na Mungu. Katika kuzaliwa kwake Mungu alituonyesha sisi uzuri, na akatufundisha kuonja na kushukuru kitu chochote kizuri. Mazingira ni nzuri na matunda ya ardhi tunayokula ni mazuri. Tunachoona angani, usiku na mchana, ni nzuri. Siku tunazoishi katika misimu, kutoka kipupwe, masika kisha kiangazi na demani, zote ni siku nzuri. Siku katika maisha ya binadamu kwa jumla ni nzuri na ni zawadi kutoka kwa Mungu.

Hizi ndizo zawadi tatu: ishi Kwa upendo, tenda mema na onja uzuri. Hizi zawadi tatu zajithihirisha katika Hadithi ya Krismasi. Krismasi ni Mwanzo mpya. Krismasi ni kuwa na furaha mpya. Krismasi ni ujumbe mpya kwa kila mtu ili tuanze Mwaka mpya tukimtukuza Mwenyezi Mungu.

Nawapongeza nyote kwa siku hizi zenye furaha. Nawapongeza kwa siku kuu ya Kuzaliwa kwa Yesu. Natoa upendo na salamu kwa wapendwa wote duniani. Nawatumia ujumbe huu kutoka Misri na kutoka kwa kanisa la Coptic Orthodox, Kanisa kuu linalotuma upendo kutoka kwa kongamano takatifu la mapadri na pia kutoka kwa mapadri wote wa makanisa ya Coptic orthodox hapa Misri. Pia natuma salamu kutoka kwa historia ndefu ambayo tunaishi na iliyo sambaa kwa makanisa yetu yote duniani. Mungu awe nanyi. Heri ya Mwaka Mpya na Heri ya Krismasi.

Papa Tawadros II